JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA

## TAARIFA KWA UMMA
## UZINDUZI WA MIFUMO NA VIFURUSHI VIPYA VYA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

***Desemba 17, 2024, Dodoma***

1. Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama (Mb) amezindua Mfumo wa Uandikishaji Wanachama, Mfumo wa Uchakataji Madai na Vifurushi vipya vya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya leo Desemba 17, 2024 Jijini Dodoma. Uzinduzi huo umefanyika ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuhakikisha Mifumo ya Serikali inasomana.

2. Mfumo wa uandikishaji uliozinduliwa unamwezesha mwanachama kujiandikisha na kujihudumia bila kulazimika kufika katika Ofisi za Mfuko. Mfumo huo unapatikana kupitia kiunganishi cha **https://selfservice.nhif.or.tz**. Aidha, Mfumo wa Uchakataji Madai umeongeza ufanisi kwa kuchakata madai kwa haraka kwa kutumia Akili Mnemba (AI) na hivyo kupunguza muda wa kufanya malipo ya madai ya Watoa Huduma.

3. Vifurushi vilivyozinduliwa ni kwa watu binafsi na familia zao ambavyo ni:-

   **a) Serengeti Afya:**Kifurushi hiki kina wigo mpana wa huduma za msingi, huduma za kibingwa na bobezi zaidi ya huduma 1,800 ambapo mchango unaanzia Shilingi 660,000/- kwa mwaka kwa mtu mmoja.

   **b) Ngorongoro Afya:** Kifurushi hiki kina wigo mpana wa huduma za msingi, kibingwa na kibingwa bobezi, huduma zaidi ya 440 ambapo mchango unaanzia Shilingi 240,000 kwa mwaka kwa mtu mmoja.

   **c) Toto Afya Kadi (TAK)**: Kifurushi hiki ni kwa watoto chini ya umri wa miaka 17 wanaosajiliwa mmoja mmoja au kwa makundi kupitia shule. Kwa watoto wanaosajiliwa mmoja mmoja mchango kwa mwaka ni TZS 150,000 ambapo watasubiri kwa miezi 3 kabla ya kunufaika na huduma. Michango ya watoto wanosajiliwa kwa makundi kupitia shule wanazosoma ni TZS 50,400 kwa mtoto mmoja. Watoto wanaosajiliwa kwa makundi, uanachama wao utaanza kwa pamoja na hakutakuwa na muda wa kusubiri.

4. Aidha, wanachama waliokuwa na Vifurushi vya Bima ya Afya vya Najali Afya, Wekeza Afya, na Timiza Afya wataendelea kupata huduma hadi muda wa uanachama wao kwenye vifurushi hivyo utakapokoma.

5. Mfuko unawahamasisha Wananchi kuendelea kujiunga na Bima ya Afya ili kuwa na uhakika wa huduma za matibabu wakati wote bila kikwazo cha fedha kupitia mtandao mpana wa zaidi ya vituo 10,000 vya kutolea huduma za afya vilivyosajiliwa na Mfuko nchi nzima.

Imetolewa na;

**Idara ya Uhusiano kwa Umma**

Jengo la NHIF Tambukareli, Barabara ya Jakaya Kikwete, S.L.P 1437, Dodoma, Simu: +255 26 2 963 888,
Barua pepe: info@nhif.or.tz, Tovuti: www.nhif.or.tz